

KISIRANI

PAKA HAWEZI KUISHI KWA MSELA

JOHN WISSE

Darohn 5 Press Tanzania Ltd,
P.O.BOX 21345,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

Darohn 5 Press Uganda Ltd,
P.O.BOX 32453,
JINJA ROAD-BC657,
UGANDA.

Darohn 5 Press Kenya Ltd,
Mombasa Road,
P.O.BOX 21345,
NAIROBI,
KENYA.

ISBN: 978-9987-9836-0-2 4

Riwaya

© 2022, Darohn 5 Press

Chapa ya kwanza, Agosti 2022

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kupiga chapa, kutafsiri au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa Darohn 5 Press Tanzania Ltd.

Wapiga chapa ni
Info tech, Malaysia

Ndani ya nusu saa nilikuwa nimenusurika kuuawa yapata mara tatu. Mara ya kwanza ilikuwa katika ajali ya makusudi iliyoua karibu nusu ya wanafunzi wenzangu wakati tunatoka shuleni. Mara ya pili ilikuwa baada ya kukoswa kugongwa kwa makusudi na gari dogo jeusi wakati navuka barabara ili nifike nyumbani kwa walezi tulipokuwa tunaishi. Ikiwa hiyo haitoshi, jaribio la tatu lilitokea nyumbani, wakati nafika. Kabla sijafunguliwa lango la kuingilia niliwaona watu wawili wakiwa wamesimama kando ya lango. Wakati nabofya kengele ili nifunguliwe, kuna watu nikawaona wananikazia macho. Kila nilipowatazama nao walitazamana wenyewe na wakawa wananong'ona.

Sikusikia walichokuwa wanakizungumza kutokana na umbali uliokuwa kati yangu na wao.

Hatimaye walianza kupiga hatua kuja langoni. Kwakuwa sura zao zilikuwa ngeni, sambamba na matukio mengi yaliyotokea, sikutaka kuendelea kuwa getini pale. Nilijiwa na wazo kuwa niondoke mahali pale. Kwa haraka mno nikapiga hatua kuelekea kwenye nyumba ya jirani zetu. Nilipofika getini nilisukuma geti dogo likawa limefungwa. Nikagonga lango na mara moja mlinzi alinifungulia. Nikaingia baada ya kuwaona wale watu wakiendelea kunifuata, na wakati naingia kwa nyuma yao kulikuwa na gari nyeusi, ileile iliyokosa kunigonga wakati navuka barabara na kuishia kumgonga bibi kizee mmoja aliyeshindwa kuona na kukimbia kwani nilikuwa nimeongozana naye.

Nilipoingia ndani nikawa ndani ya kibanda cha mlinzi. nikachungulia nje. Huko nikaona watu wale wasiojulikana

wakisimama mbele ya geti na kujadili jambo, ila wakaondoka mara tu baada ya ile gari kusimama na wao kupanda. Wakati wanaondoka niliona yule mwanamke mrefu, mwembamba na mweusi akipiga picha eneo la nyumba ile nilikuwa nikiishi.

Moyo wangu ulikuwa kasi mno ukipiga, lakini nikajikuta nashusha pumzi kwa nguvu baada ya watu wale kuondoka.

Bawabu wa nyumba ile muda wote alinikazia macho na asijue kilichotokea. Nilichokiona na kukihisi sikumweleza waziwazi. Lakini kwakuwa ilikuwa si kawaida yangu kuingia kwa dharura mahali popote, basi ilikuwa lazima kwa mlinzi yule kuniuliza. Kweli akauliza, "Kuna nini Jamshid?"

Nikatingisha kichwa tu na kumjibu, "Sijui."

"Hao akina nani?" akauliza tena.

Nikamjibu, "Sijui."

Bawabu akabakia kimya kwa sekunde chache. Akawa anatafakari. Nilimtazama usoni kwa ujasiri kwani nilikuwa namfahamu vilivyo. Hatimaye bawabu yule nikamuuliza, "Mkumbo, mwenzako yuko wapi?"

"Nani?"

"Sewando, mlinzi wetu pale getini?"

"Hayupo."

"Nimebisha hodi na kubofya kengele, siitikiwi wala. Hakuna anayefungua. Si kawaida yake...." nikaeleza wasiwasi wangu.

"Mh!" akaguna.

"Hujamwona tangu asubuhi?"
nikamuuliza.

Mkumbo akavuta pua zake na kulipakata gobole lake kwa kulipachika kifuani. Akazungusha domo lake kushoto na kulia kisha akatema rojo la mate ya ugoro uliokuwa mdomoni mwake. Akayasukuma mate yale kwa mguu wake wa kushoto na kuyatimuatimua akiyachanganya na

mchanga uliojazana pembeni ya ukuta ulizunguka nyumba ile. Mkumbo akapiga hatua kuelekea upande unaopakana na nyumba yetu. Akaita kwa nguvu, "Sewando!"

Kimya kikatawala.

Akarudia tena na tena kuita, bado hakisikika Sewando wala yeyote akiitika kutoka ndani ya uzio wetu.

"Au amefukuzwa?" Niliuliza kwa mashaka.

Mkumbo hakunijibu.

"Wazazi wangu je, uliwaona wakienda kazini leo?"

Mkumbo akatafakari ili akumbuke. Akabakia bubu, ila akanitazama usoni tu kama ni mwenye mashaka.

Sikutaka kupoteza wakati na Mkumbo. Nilitoka na kueleke getini kwetu ambapo nilijaribu kusukuma mlango mdogo. Bado ulikuwa mgumu. Haukufunguka.

Niliita mara kadhaa lakini ukimya ukawa uleule.

Sasa nikajiwa na wazo kuwa niligonge geti kwa nguvu ili angalau mbwa wetu Shilata asikie na apige kelele kutokana na usumbufu ule. Huenda Sewando niliyedhani amelala angeachiwa na usingizi. Hata hivyo kelele zangu zikawa za bure. Sikumsikia Shilata wala Sewando akiitikia mwito wangu.

Nafsi iliyonusurika kifo mara kadhaa ikafurikwa hofu. Hofu ya kufa ikatanda lakini nikajitahidi kuizuia. Nikauvaa ujasiri kwa kulivua begi langu la mgongoni na kulirusha lipite juu ya ukuta kisha liangukie ndani ya uzio. Niliposikia kishindo cha begi langu ndani ya uzio nami niliuparamia ukuta. Nikakwea kama paka na nikatambaa taratibu kuushuka nikiwa upande wa ndani. Umbali ulipobakia mfupi niliamua kuruka na kutua kwenye sakafu ya vijitofali vya seruji. Nikaangaza macho huku na kule nigali nimechutama bado. Sikuona mtu

kwenye uga wote wa nyumba yetu. Sikukumbuka kulichukua begi zaidi ya kuelekea kwenye mlango mkubwa wa kuingili ndani kwetu. Mlango ulikuwa wazi. Niliusukuma ukakubali kufunguka.

"Sewando!" niliita.

Kimya kikawa kwa maana hakuna aliyeitikia.

Nikaita tena, "Mama!"

Kimya!

Nikaita mwingine, "Baba!"

Kimya!

Nikakumbuka kumwita dada yangu, "Dada Zuu!"

Kimya!

Hakuna yeyote aliyeitikia. Nikaingia sebuleni ambapo sikuona chochote zaidi ya masofa na meza yake ikiwa imetulia katikati ya sebule. Niliangaza macho pale sebuleni nikaona peupe tu. Masofa yalitandikwa kwa vitambaa vya pinki, vyenye duara la maua ya kijani.

Kwa jinsi nilikuwa nakiheshimu chumba cha wazazi wangu sikutaka kuingia huko kwanza. Nilielekea kwenye chumba cha dada yangu Zuu, ambaye alikuwa kamaliza mitihani ya kidato cha nne na matokeo bado yalikuwa hayajatoka. Kwakuwa chumba chake kilikuwa karibu na ukumbi wa kupumzikia, nilikifikia cha kwanza. Hapakuwa na mtu chumbani. Nikaiona picha yake kubwa ikiwa ukutani naye akiwa katabasamu katika joho la sherehe ya kuhitimu masomo. Picha ile dada Zuhura aliipiga wakati wa mahafali yake.

Nilipojaribu kupekua chumba chake kwa macho niliona kama kila kitu kilikuwa sawa. Nikarudi sebuleni ili nipige simu kutaka kujua walipo.

Simu ya mezani ilikuwa haitoki kwa maana haikuwa na mawasiliano kabisa. Nilipoitekenya mara kadhaa ili nisikie kijimlio cha kuniweka sawa kuingiza namba, sikukisikia, badala yake nilisikia kama mvumo wa upepo katika mwambao wa

bahari. Nikaja kubaini kuwa, simu ilitenganishwa na mkongo wa mawasiliano.

Ghafiliko likawa kubwa nafsini na kufanya niachane na simu na sasa nielekee mahali kwingine.

Nilikivamia chumba cha wazazi wangu, nako hakukuwa na mtu yeyote. Kitanda kikubwa chenye nakshi za kiajemi kilikuwa kimetandikwa sawasawa na kila kitu kilikuwa mahali pake. Chandarua cheupe kilikuwa kimekunjwa vizuri na shuka jeupe lilishikana na godoro sawasawa na kuliacha ua jekundu la waridi likitanda katikati yake. Lakini ndani humo palikuwa kimya, hakuna mtu wala dalili ya yeyote.

Sikuenda chumbani kwangu, ila sasa nilielekea nje ya nyumba, kuliko na banda la mbwa wetu, Shilata. Huko sikuweza kuhimili wimbi la hofu iliyonivaa. Shilata alikuwa sakafuni mwa banda akiwa katulia. Mdomo ulikuwa wazi na nilipomshika mwili wake tayari ulikuwa mzoga. Alikuwa ameshakufa na alikauka kabisa.

Kengele ya hali ya hatari ilinijua kuwa hapakuwa na usalama mahali pale. Nikarudi ndani mwetu ili kufanya jambo. Kwenye kamera ya riri iliyofichwa na mapambo ya nyumba ndipo kukawa kimbilio langu ili angalau nione kilichokuwa kinaendelea. Kamera ile iliunganishwa vizuri na kioo chake kilicho kama runinga ndogo ambapo nilikuwa na uwezo wa kurejea taarifa za matukio yote yaliyopita kwa muda wote niliokuwepo.

Sasa nikawahi kwenye kile kijiruninga kidogo cha CCTV Kamera. Nikabonyeza ili kiwake. Ah—wapi! Hakikuwaka. Nikatumia nguvu kubonyeza kitufe ya kukiwasha lakini wapi, hadi vidole vyangu vikawa vinauma. Baadae ndo nakuja kubaini kuwa, hapakuwa na umeme nyumba nzima.

Nilichomoa kadi iliyokuwa inahifadhi kumbukumbu za matukio yote na kuitia kwenye nailoni. Sikutaka kupoteza muda kwani tayari nilijua kuna watu walikuwa njiani wakiniwinda. Uamuzi wangu

ulikuwa kwanza niende nje ya nyumba kabisa ndipo nianze taratibu za kujua ukweli. Nikaamua kuingia chumbani kwangu ili nibadili nguo.

Nilipousukuma mlango ili niingie, nikajikuta napigwa na wimbi la mshtuko. Macho yakabakia wazi. Mdomo nao wazi huku mwili wote umepigwa ganzi na natetemeka kama mwenye kupigwa mkondo wa umeme. Nikahisi baridi kali lakini jasho jembamba nikalihisi kutambaa kwenda nyayoni. Nilikuwa mwepesi wa kulia lakini sikuweza kutokwa chozi kwa jinsi kiliniumiza kilichotokea.

Hamadi! Jicho halina pazia tu, wala nisingetaka kuona. Moja kwa moja nikashuhudia familia yangu yote ikiwa chumbani kwangu. Baba alikuwa sakafuni kalala katika biwi la damu. Bawabu wetu alikuwa sakafuni pia, shingo yake ilinyongotwa hadi ulimi wake ukashindwa kusitirika kinywani. Mdogo wangu wa kiume Pinto alikumbatiana na mama

kitandani. Mama alikuwa juu ya Pinto kwa maana alikuwa anamficha. Kulikuwa na kisu kilichozama mgongoni kwa mama na damu zilikuwa zimeacha kutoka. Lakini kati yao, sikumwona Zuhura pekee ili idadi ya watu wafamilia yangu wakamilike kwa idadi.

Nilihisi kumwona muuaji akinijia katika fikra zangu. Nikahisi watu wale waliokuwa wakinifuatilia walikuwa ndani na walingoja sekunde chache tu nami wanimalizie. Hakika niliogopa sana.

Nilitoka mahali pale nikiwa mkuku na moja kwa moja nikaelekea ulipo mlango. Nilijikuta nipo getini nikihangaika kufungua. Pamoja na juhudi zote, geti lilikuwa limefungwa kwa ufunguo, hivyo nikashindwa kutoka. Muda huo ndipo nikasikia ngurumo ya gari nje ya geti na mgongano wa funguo ukafuatia baada ya injini ya gari kuzima. Nikachungulia kwa chini. Nikaona mtu aliyevalia buti za jeshi

zilizojaa tope, tena hazitamaniki. Moyo ukachachawa na nikahisi kupoteza fahamu.

2

Mwanga wa jua la asubuhi ulijipenyeza kwa fujo na kujaa chumbani nilimokuwa. Macho yangu yakiwa yamepigwa upofu sikuwa na uwezo wa kufikiri vizuri. Sikujua mahali nilikuwa hadi wakati ambao wimbi la harufu ya kemikali za hospitalini lilipozifikia pua zangu. Nilipoihisi harufu ile ya madawa ndipo nikafumbua macho ili nipate kujua kinachoendelea.

Kabla sijabaini kuwa mahali pale ni sehemu gani, nikasikia sauti za kunguru wakizogoana. Fikra za kuwa pale ni hospitali zilikuwa bado kunijia. Ila nikawa na wasaa wa kuruhusu macho kufunguka. Nikaanza kujikusanyia mwanga na kuufanya uendane na nuru ya macho yangu. Lakini wakati ule kichwa kilikuwa kinauma

bado. Taratibu nilipofumbua macho, nikaanza kuyasoma maandishi yaliyokolea kwa weusi katika shuka. Nilikuwa katika moja ya wodi katika hospitali ya Mwananyamala, katika jiji la Dar es salaam.

Mkononi nilikuwa na *kanyula* ambayo ilikuwa ikiendelea kunimiminia tiba ambayo sikuwa najua ni ya nini.

Hatimaye katika tafakari zangu nikasikia sakafu ikilalama—ko, ko, ko, ko! Nikanyanyua uso wangu ili nione aliyekuwa anakuja kwani kitanda changu kilikuwa mkabala na mlango wa wodi. Wakati natazama kwa kulazimisha kuona mbele ndipo nikabaini kuwa sikuwa na uwezo wa kuona mbali sawasawa. Niliona winguwingu la kijivu zaidi. Nilihisi mahali ni pazito, hasa sehemu ya paji la uso wangu. Nilipopapasa, kwenye paji langu la uso palikuwa na kidonda, na palifungwa bandeji ambayo niliihisi baada ya kupagusa. Hangaika yangu ikanifanya nihisi maumivu

makali hata nia ya kutaka kumjua aliyekuwa anakuja ikawa imetoweka.

"Endelea kupumzika, na usiendeleo kutaka kutazama. Itoshe kwa sasa kusikia tu," alisema mwanamke ambaye sasa nilihisi kuwa ni muuguzi.

Bado nikasikia hatua zake kunifikia nikiwa nimefumba macho.

Nikamuuliza, "Kwani kuna nini? Na hapa je?"

Akaniambia, "Ulipata ajali...na aliyekuleta hapa ni mtu aliyekusababishia hiyo ajali."

"Nani?" nikauliza.

"Hata simjui...ila ni mtu wa serikali. Alipokuleta hapa alisema alikugonga na gari, mengine siyajui."

Nikastaajabu sana kusikia kauli hiyo. Kila nilipojaribu kuwaza ili nikumbuke, sikuweza, zaidi kichwa kiliuma zaidi. Nikabakia kimya navuta kumbukumbu iliyopotea.

"Kwa sasa hupaswi kabisa kuumiza kichwa chako kwa mawazo. Utazidi kuumia zaidi. Naamini kwa tiba uliyoipata, kama utaendelea hivi, Nina hakika kuwa ndani ya mwezi mmoja utanza kufanya mazoezi," akasema yule muuguzi.

Maneno yale yakanishtua maradufu. Nikataka kunyanyuka lakini nikashindwa. Muuguzi yule akaja haraka sana na kunizuia akitaka nisinyanyuke kutoka mahali pale. "Nielewe wewe mtoto. Hupaswi kuusumbua mwili wako kwa lolote. Hata kama unataka kwenda haja ndogo nitakupeleka ila usifumbue macho yako kwa muda mrefu, wala mwili wako hauna nguvu za kwenda mahali peke yako. Chochote utakacho niambie nikusogezee."

Kauli ile tena ikanifanya nijitathmini upya. Nilikuwa nimevunjika mguu mmoja sehemu ya paja. Mkono wa kushoto uliteguka sehemu ya bega. Akaniambia pia kuwa, damu ilivilia kwenye ubongo na tayari madaktari walishanifanyia upasuaji

kwa mafanikio makubwa. Sikuwa na swali tena zaidi ya kusinyaa katika kitanda changu.

Kweli muuguzi yule ambaye baadae nilikuja kumtambua kwa jina lake akiitwa Bupe alinihudumia kwa kila ambacho mwili wa mgonjwa ulitaka kuhisaniwa. Akawa ananibembeleza na kunifuta machozi.

"Ukipona utarudi nyumbani.." akasema.

Maneno yale yakanirejesha mbali. Yakanivutia kumbukumbu iliyokuwa imeenda mbali. Kichwani likaja wimbi la picha za kumbukumbu. Likaja wimbi la vifo nilivyoshuhudia ndani ya chumba changu. Nikakumbuka nilichokuwa nimekiona mara ya mwisho kabla sijapoteza fahamu.

Niliona Marehemu! Nikawakumbuka wafu ambao ni wazazi wangu, mdogo wangu na bawabu wetu. Nilipasuka kwa kilio kilichojaa wodi nzima. Sikuwa nahitaji chochote ila nilisimama kwa kulazimisha. Nikataka niondoke na kwenda. Muuguzi alipoisikia sauti ile kali alifika na wenzake

wengi wakiwa mbiombio. Wakashirikiana kwa pamoja kunishika na kunilaza kitandani. Daktari mmoja akashauri nifungwe mkanda kushikizwa kitandani ili nisiwasumbue tena.

Kweli wakanifunga.

"Mchome sindano ya usingizi haraka!" alisema daktari wa kiume aliyekuwa kajawa ghadhabu nafsini. Alikuwa akiongea kwa sauti kali iliyoonesha wazi kuwa ni mwenye kujawa hasira. Kama ilivyoagizwa, nilichomwa sindano katika mshipa wangu mkubwa wa mkononi. Sikuweza kujitetea kwani tayari mkanda ulinishikilia. Maumivu makali ya dawa iliyokuwa ikisambaa mwilini mwangu niliyahisi waziwazi. Dawa ile ya usingizi ilinichukua kwa muda mfupi sana. Nikajikuta usingizini.

Siku za kubaki pale hospitalini kama Bupe alivyonielea kuwa nitakuwepo kwa mwezi mzima ndipo niruhusiwe zilimalizika nikiwa nje ya hospitali ile. Sasa nilikuwa nimefichwa shambani kwa Bupe, nje kidogo ya jiji la Dar es salaam. Hali yangu ilitengemaa na nikawa najihisi mwenye nguvu za kutosha. Bupe alinitorosha kutoka hospitalini baada ya kubaini kulikuwa na njama za kuniua.

Kwa mujibu wa maelezo yake alisema kuwa, kuna watu walijaribu kuingia wodini kwa siri ili waniangamize. Alinipatia ushahidi mbalimbali na ndipo nilitumia muda wangu kumsimulia. Nilimweleza kila kitu kilichotokea katika familia yangu. Bupe ndipo alichukua uamuzi wa kunipeleka katika shamba lake huko Chanika.

Sasa ilikuwa saa kumi na moja jioni. Nilikuwa namalizia kulisha kuku wake aliowafuga akitaka kuniondolea upweke kwa kuwa nawahudumia kuku. Siku hiyo nilikuwa namtarajia Bupe kuja kadiri ya

tulivyokuwa tumekubaliana. Hadi wakati jua linaficha makucha yake, sikuiona gari ya Bupe ikija, ila nikaliona gari jingine tu jeusi likija na kupitiliza kwa mita chache tokea nilipokuwa. Nilijiwa wasiwasi. Dhana ya kuwa huenda watu wale wakawa na nia mbaya ilinifika tu nafsini nikajikuta nachukua hadhari.

Kwa kuwa gari ilikuwa usawa wa mlango, mbele ya nyumba, nilijikuta nafsini napata njia ya haraka ya kutoroka. Niliingia ndani mara tu nilipoona kioo cha upande wa kulia wa gari lile kikishushwa na nikazona sura za watu ambao sikuwa nawajua. Kwa kila hali walikuwa na mwenyeji wakielekezana mahali niishipo.

Nilipoingia ndani nilielekea chumbani. Kulikuwa na dirisha dogo la mraba ambalo lilikuwa na ukubwa wa kuweza kupita mtu mwenye umbo kama la kwangu. Nilichupa hadi pale nikajivuta kama paka na kupenyeza kichwa changu katika dirisha hilo. Nikatoa kichwa nje kisha kujivuta

kama joka na kuchomoa kiwiliwili. Nilichupia nje na kuambaa kwenye shamba la mihogo lililokuwa limetanda upande wa nyuma ya nyumba.

Wakati naingia shambani na kujibanza mahali palikuwa na mnazi mchanga uliochanua matawi yake, nilisikia kishindo kikali. Bila shaka walikuwa wakiuvunja mlango ambao nilipoingia ndani niliufunga kwa komeo. Tayari nilijua wakati ule ulikuwa wa kujiokoa.

Mbio zangu zilizojaa mauzauza zilinichukua hadi katikati ya shamba. Ndipo nilisikia ngurumo ya gari ikisikika upande wa pili wa shamba la mihogo. Bila shaka walikagua ndani wakanikosa, ndipo wakaona dhahiri nilipopita pale dirishani. Nilijua wangebaini hilo kwani niliacha alama ya nyayo zangu mahali nilichupia. Eneo lile lilikuwa na mchanga mwingi uliorundikwa na ulikuwa mbichi bado ukingoja shughuli za ujenzi.

Sasa nia ya kuwatoroka ikazidi kufifia. Miale ya jua la jioni ikiwa imekazana kunichoma ndivyo damu yangu ilizidi kuchemka. Ndivyo moyo wangu ulizidi kuchachawa na kulia kwa huzuni. Kila mara nilijiwa na wimbi la wafu waliokuwa katika chumba changu. Nilipokuwa nimechutama nikawa naweza kuona kupitia mashina ya mihogo. Nikaona miguu yenye viatu vyeusi ikikazana kupiga hatua kuelekea ndani ya shamba nilimokuwa. Waliamua kunizingira kwani wenye gari walizunguka upande ambao nilitaka kupitia na kuepa. Nilikuwa nimewaza nikilimaliza shamba la mihogo ningeweza kuingia kwenye shamba la michungwa la jirani yetu. Tokea hapo ningeshika kichocho ambacho kingenipeleka hadi sehemu wanayoiita Msumbiji--mahali ambapo pana soko la mazao ya shamba ningeweza kudandia gari na kutokomea mahali kwenye usalama.

Nikiwa nimebabaika, fikra zangu zikabishana na kuniyumbisha huku na kule.

Upande mmoja ukaniambia, *simama wakukamate!* Upande mwingine ukabisha kwa nguvu, ukaniambia, *kimbia huku ukipiga kelele ili watu wakusaidie.*

Yote hayo niliyapuuza, nikawaza kinyume chake. Nikajiwa na sauti ambayo sikujua ilikotokea. Ikanieleza, *tazama upande wako wa kulia. Tazama! Tazama!* Nikageukia upande wa kulia kwangu wakati ambao vishindo vya wawindaji wangu vikiwa karibu yangu. Nikawa nasikia matawi ya mihogo yakivunjika pa, pa pa! Kulia kwangu baada ya kupageukia nikaona kisima ambacho kilikuwa hakijaanza kutumika bado. Kilikuwa kisima ambacho Bupe alikuwa akikichimba. Siku hiyo mafundi hawakuwa kazini, na kila kitu kilikuwa mule ndani. Kilikuwa kimejengewa tayari na kutiwa mfuniko kwa juu. Hapohapo nikasikia tena sauti ikinihimiza, *Nenda! Nenda kaingie kisimani.*

Nilijivuta haraka mno kama nyani. Niliushika mfuniko wa kisima kile

nikaufungua. Mfuniko ule ulikuwa sawa na dirisha nililopita wakati natoroka nyumbani. Nilipofungua nikasukuma mboni yangu kuona ndani ya kisima lakini nikaishia kuona giza tupu. Sikujali tena maana nilikuwa nimeshaona tayari uwemo wa ngazi iliyokuwa ikitumiwa na mafundi wale wakati wa kuingia na kutoka. Ili kuwapoteza uelekeo adui zangu niliokota jiwe mahali pale nikalirusha. Lilienda upande wa pili uliokuwa na minazi michanga likapiga majani na kuzalisha kelele. Mimi muda huo ndipo niliingia haraka mno kisimani na kuuruhusu mfuniko kujifunika pasipo kupiga kelele. Macho yangu yakabakia kutazamana na giza ndani ya kisima kile.

Masikio yangu bado yalikuwa yamekita kambi nje yakisikiliza kila kitu kinachotokea. Nilichosikia ni vishindo kisha nong'ono ya watu wakinong'ona jambo. Sikuwa nasikia walichokuwa wakizungumza. Ilikuwa dhahiri kuwa watu wale walikuwa juu ya

kisima kile. Nilijiweka tayari kumvuta yeyote ambaye angejaribu kuufungua mfuniko ule kwani ilikuwa lazima aonje mauti.

Nafsi yangu ilifubaa huku moyo ukijaa ujasiri wa kuua yeyote. Nilikuwa kama paka aliye katika hatari ya kuuawa na kundi la mbwa. Nikatamani kutoka katika giza lile nikapambane na watu wale, ila ikaja sauti kunikemea juu ya uamuzi huo. Nikajikuta natulia baada ya kujiwa na santuri ya sura za wafu wa familia yangu ile changa.

Ulipita muda, takribani dakika kumi na tano nikiwa nasikia vishindo na hali ya taharuki katika shamba. Bila shaka walikuwa wakinisaka kila kona na hawakuamini kuwa nilitoroka na kwenda nje ya shamba lile.

Nikiwa nawaza kuwa kimbunga kile kimepita, nilisukuma mfuniko na kuchungulia kama nguchiro. Sikuona mtu, wala sikusikia kishindo chochote cha kuogofya. Nikaamua kutoka ili niondoke na

kwenda mbali zaidi. Nilipoangaza macho yangu kulizunguka shamba, sikuona mtu wa kutilia shaka kabisa. Tayari ilikuwa inaelekea machweo.

Lahaula! Sikujua wala sikuota kama watu wale waliweka mtego mkali ili kuninasa. Baada ya kukipa kisogo kisima kile, kumbe kuna mwanaume mmoja aliachwa kama mlinzi. Alikuwa kapanda kwenye mti wa mpera uliokuwa ndani ya shamba lile la mihogo. Kwanza nilisikia kishindo katika eneo la mpera. Nikasimama haraka mno na kutazama mahali kule. Kilichofuata nikasikia vurumai, matawi ya mihogo yakilalamika. Nilipochunguza nikamwona mwanaume mrefu, mweusi akiwa kavaa fulana jeusi, lenye mikono mirefu. Suruali yake ilikuwa na mabakamabaka ya jeshi. Niliduwa mahali niliposimama nikawa kama nimenaswa na sumaku. Nikamkazia macho naye hakujali matawi ya mihogo kuwa yalimzuia. Aliponikaribia nikajikuta ghafla mno

nabadili fikra. Nikanyanyua mguu na kuanza kupiga hatua nikimkimbia.

"Simama, wewe nyani!" alinionya.

Sikutii sauti yake. Nikaongeza kasi wakati nakimbia.

Niliruka matuta kadha wa kadha akiwa nyuma yangu ananifuata. Mkono mmoja alikuwa kashika bastola na mkono mwingine ulikuwa na simu. Kila nilipotafakari kuhusu mahali niliiona sura ile sikukumbuka, ila wakati naendelea kukimbia ndipo nilijiwa na wimbi la kumbukumbu. Mwanaume yule ni miongoni mwa watu wawili niliowaona wakinifuatilia siku wazazi wangu waliuawa. Ndiye alikuwa kaongozana na mwanamke wakati nagonga geti nikitaka kufunguliwa, na baada ya kuona sifunguliwi nikaelekea kwa mlinzi wa nyumba ya jirani. Napo walifika na wakatoweka bila kujua walikoelekea.

Nilipofika usawa wa kisima niliinama na kuuvuta mfuniko ili niingie ndani.

Akanionya, "Umeshachelewa. Tulia kama ulivyo usalimike, ama nikufyatulie risasi kisha nikuzike ndani ya kisima hicho asiwepo hata wa kuona maiti yako."

Nilimtazama akiwa anakazana kupiga hatua kunijia. Bastola yake nikaisikia inalegeza maungo akiruhusu risasi kuwa tayari kwa shambulizi muda wowote. Mkono wa kushoto ukiwa bado umeshika mlango ule wa kisima, kulia nilishika jiwe kama silaha yangu ya kujihami. Lakini baadae nikajiwa ujasiri wa kuzama kisimani na kuufunga mlango. Nilibana mahali si mbali na mlango nikiwa nimeikanyaga ngazi ile kwa ujasiri.

Mwanaume yule nilijua kuwa lazima angeinama na kufunua mfuniko bila hata kuchukua tahadhari kwa vile nilikuwa dhaifu kwake. Kwanza nilisikia akicheka na kutoa maneno ya kejeli kuwa, "Sungura mchanga karudi tunduni."

Alipoufungua mlango na kuchungulia nilimsukumia lile jiwe nililokuwa nalo

mkononi. Ni wakati uleule nilimvuta na kumsikia akijibamiza kwenye ngazi kisha kwenye vyuma vilivyokuwa vimesimikwa ndani ya kisima kile. Mwisho nilisikia vurumai ya mtu kutua chini ya kisima kulikokuwa na maji. Sikutaka kujua kilichompata, ila nilitoka haraka nikaufunga mlango wa kisima. Katika komeo nikachomeka mti kuzuia harakati yake yoyote akitaka kujinusu.

Sikuwa na kituo. Sasa nilitimka mbio na kwenda kwenye mti wa mnazi uliokuwa kando ya shamba. Nilitazama kila upande na sikuona mtu ndipo nikafukua na kuuchomoa mfuko wa nailoni niliokuwa nimeuficha. Mfuko ule ulikuwa na kadi ya kielektroni iliyorekodi matukio yote ya siku zile ambazo wazazi wangu walishambuliwa. Niliamini kadi ile ingeniwezesha kuwajua wauaji na ndipo ningechukua hatua kali kulipa kisasi.

Niliusokomeza mfuko ndani ya kaptula yangu na kuanza kutimka mbio. Baada ya

mwendo mrefu katika kiza kile niliona ni vema nikatafuta mahali pa kuficha ile kadi ya matukio kutoka katika kamera yetu. Nikajiwa hofu kuwa huenda nikanaswa, na pengine wanaonisaka walishatambua kuwa nilinyofoa kadi ile kwa ajili ya ushahidi utakaowafanya waingie hatiani. Hivyo nilienda moja kwa moja katika jumba ambalo lilikuwa linaendelea kujengwa. Kwanza ndo kulikuwa na kenchi juu na halikuwa limeezekwa bado. Nikavuka sebuleni na kuingia kwenye chumba kimoja cha jengo lile. Lilikuwa bado halijatiwa sakafu hivyo kulikuwa na vumbi jingi na madongo laini.

Katikati ya chumba nikapapasa na kupata pande la ubao na kuchimba shimo ambapo niliuzika mfuko ule. Niliondoka na kuanza kutafuta mahali salama zaidi kwangu.

3

Baada ya miaka mitano

Takribani miaka mitano ilipita nikiwa sijachomoza sura yangu katika jiji la Dar es salaam. Miaka yote tangu nitoroke nilikimbilia Mwanza. Kwa miaka yote hiyo, kila mara nilikuwa nikishikwa msukumo wa kutaka kurudi jijini Dar es salaam ili angalau nipate kujua kilichokuwa kinaendelea baada ya wazazi wangu kuuawa. Kila mara nilipowaza kufanya hivyo nilijiwa sauti ya kemeo. Sauti hiyo ilinitaka kutojaribu kusogeza pua yangu huko kwa hofu kuwa nitatiwa mbaroni na wauaji ambao sikuwa na jua sababu iliyofanya wapendwa wangu kuuawa.

Kila mara nilikumbuka kuwa nikaichukue ile kadi na kuwapelekea polisi ili kama wauaji watabainika wakamatwe na

sheria ichukue mkondo wake. Napo nilijionya kwa hofu kuwa, huenda polisi wakanihujumu kwa maana sikuwa na yeyote wa kusimamia shauri lile, pengine wauaji wangejua hilo wangenifuta tu mara moja kwa risasi na ushahidi utoweke.

Niliwaza ni mahali gani walikokuwa ndugu wa baba au mama yangu—kwa hali ilivyokuwa, sikuwa namjua ndugu yeyote. Tangu nizaliwe sijawahi kuona ndugu zake baba wala mama wakija jijini kututembelea japo kuna wakati nilisikiasikia fununu kuwa walikuwepo. Wazazi wangu hawakutuonesha waliko ndugu hata tukajuana.

Kila nilipowaza hayo nilijipa moyo kuwa muda utafika na haki yangu nitaipata Utafika muda wa kuwatafuta wauaji mimi mwenyewe nikiwa mkubwa, kwani niliamini kuwa kadi ile isingeweza kupotea kwa namna yoyote. Kama ni kuingiwa na vumbi isingewezekana; kama ni maji pia isingewezekana; kama kuokotwa napo

isingeokotwa na yeyote; hata kama moto ungezuka—hakika nilikuwa nayo kuwa kadi ile isingepatwa na tatizo lolote kwakuwa niliificha kwa kuichimbia.

Kwa kipindi chote cha miaka mitano sikuwa nimemsimulia yeyote kuhusu tukio lile. Japo maisha yangu kwa kiasi kikubwa yalikuwa katika stendi ya Nyegezi, mahali pale sikudumu. Nilikaa muda mfupi katika stendi ile na wabangaizaji wenzangu. Nilipata rafiki wengi waliokuwa wakiishi kama mimi, ila wawili pekee ndio walikuwa wa kufaa. Tulifanana kwa kila hatua kuwa wao hawakuwa na wazazi, nami nikiwa sina wazazi na sikujua chimbuko la familia ya wazazi wangu.

Tuliamia mkoani Mara baada ya maisha katika stendi kuwa ya mashaka. Kila wakati tulikamatwa na polisi kutokana na watu kututuhumu kuwaibia ama kuwabughudhi na tulipelekwa kituo cha polisi ambako tulichalazwa viboko na kudhihakiwa mno. Kuna wakati tulipewa

kesi zisizofaa ambazo zilipelekea kukaa gerezani kama mahabusu na mwisho mahakama ilituachia kwakutokuwepo kwa ushahidi.

Japo nilikuwa katika maisha yale ya dhiki, sikutaka kabisa kuhusishwa na uhalifu wa aina yoyote. Sikupenda sana kufanya dhuluma ama kujipatia riziki kwa jasho la mtu mwingine bila yeye mwenyewe kuhiari kunipatia. Nilinua kujilea mwenyewe—kwa nguvu na akili zangu. Tulipohamia mkoani Mara moja kwa moja tulijipatia makazi katika makambi ya wachimba migodi. Ni mahali ambapo watafuta riziki kwa kutegemea madini waliweka kituo wakijaribu mara kadhaa kutafuta vibarua vya uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Hata sisi tulifanya vibarua vya hapa na pale—kama kubeba viroba vya mchanga na kuwapelekea wachenjuaji, ama kushiriki moja kwa moja katika uchenjuaji kwa kutumia kemikali ya zebaki katika makarai.

Jambo baya zaidi lililoibuka kadiri siku zilivyozidi kwenda mahali kule ni kufanywa watumwa kwa sababu ya dhiki. Kuna wakati ambapo tulikosa kabisa vibarua tukawa tunashiriki katika kazi ya wizi. Ilikuwa kazi ya kujipenyeza kwa siri hadi ndani ya mgodi kwenda kuiba mchanga wa dhahabu kwa malipo yasiyo na tija. Malipo ambayo yalilenga kushibisha matumbo yetu pekee.

Hali ile niliihimili kwa mashaka mno kwani muda wote nilikuwa roho mkononi kwa woga wa kuuawa. Kila nilipokuwa katika eneo la mgodi wakati wa kuiba viroba nilihisi kushambuliwa kwa risasi na walinzi wa eneo lile. Pale ndipo nilijiwa na kumbukumbu mbaya ya familia yangu niliyoishuhudia ikiwa imemalizwa kwa risasi na kisu.

Tuliendelea na tabia hiyo ya kuiba mchanga na kwenda kuwauzia waliotutuma hadi arobaini zetu zikafika siku moja. Siku ya kukamatwa ilikuwa usiku wa mvua

kubwa iliyoanza kunyesha wakati wa jioni. Iliendelea hadi machweo. Usiku ulipokomaa tuliongozana na wenzangu hadi nyuma ya mgodi, sehemu ambako kuna mitambo ya kuchenjulia mchanga wa dhahabu. Kulikuwa na mifuko kwa mamia ikiwa imebebana ikingoja kuchenjuliwa kwa vinu vya kisasa vya kunasa dhahabu. Huko nilikuwa wa kwanza kuingia kisha wakafuata rafiki zangu wawili. Wakati tunaingia palikuwa kimya, ila manyunyu yaliendelea kunyonyota na kulikoa bati lililoezekwa na kuhifadhi mitambo pamoja na shehena ya mifuko ile yenye mchanga uliomeza dhahabu.

Kabla ya kuingia tulikuwa tumechana fensi kwa mkasi wa kukatia vyuma. Tukaelekea kwenye banda lililokuwa na mchanga wenye dhahabu uliotoka chini ya ardhi na kuhakikiwa. Moja kwa moja niliwahi ili nikachukue kiroba changu kisha niwe wa kwanza kutoka kwa usalama zaidi.

Lilitokea jambo la kustaajabisha sana, tena jambo ambalo hatukulitarajia. Kwa ghafla mno taa kubwa za ulinzi zilitapika mwanga mkali uliotuanika. Kwanza nilikuwa ndo nimekishika kiroba cha mchanga wa dhahabu ili nikivute na kukitupia begani.

Mwanga ulipojaa nilihisi kuwa nipo uchi. Moyo wangu ulisimama kwa sekunde kadhaa kwa sababu ya hofu iliyokuwa imenijaa. Nikauhisi mkojo unatiririka kufuata mapaja yangu na kutua chini ya nyayo. Nyayo zangu wakati ule zilikuwa zimemezwa na tope la mgodi kwani eneo tulilojipenyeza lilikuwa oevu na ndipo mahali pekee mchanga uliochenjuliwa na matope yote ulitiririshwa kama ujiuji baada ya kuoshwa. Hivyo palikuwa na tope lililomezana na kemikali ambayo ni hatari japo hatukuiona hatari kama tulivyoiogopa njaa.

Mlio wa tahadhari ulisikika kwa king'ora na nikaona eneo linazingirwa na walinzi wa

mgodi ule. Nilifumba macho na kufumbua huku jasho jembamba likiwa linashindana kutoroka mwilini kwangu. Nikawa siwezi kupiga hatua kwenda popote zaidi ya kusimama. Hatimaye taa zote zikaelekezwa mahali tulipo. Nilinyanyua mkono wa kulia kisha ukafuata wa kushoto, yote ikawa juu. Nilitii amri iliyotolewa na walinzi kuwa tujisalimishe. Sikujali hali mbaya ya mahali tulikuwa. Nilifutika magoti katika tope lile ingali mikono yangu ipo juu kwa kutii amri.

Walinzi walipotufikia walitufunga kamba. Nilikuwa wa kwanza kufungwa kamba baada ya mikono yangu kurudishwa nyuma. Mlinzi mmoja nikasikia anasema, "Leo tumewanasa. Kwa kipindi kirefu mmehatarisha ajira zetu—leo mtajuta."

Tulisukwasukwa na kupelekwa kwenye ofisi ya walinzi wa mgodi ule. Mtu mmoja aliyeonekana kama mkubwa wa kundi lile la walinzi alipiga simu kwa polisi.

"Afande, tuma vijana wako hapa katika lango la mgodi, kuna wezi tumewanasa."

"Hatuna gari!" ilisikika sauti upande wa pili. "Washikilie hadi asubuhi magari yatakapotoka doria tutakuja kuwachukua," alisema polisi.

"Sawa afande!"

"Lakini...eh..ni wakorofi labda? Wako wangapi?" aliuliza askari katika simu. Ile hali ya ukimya na utulivu wa anga ilifanya tusikie kila neno.

Sote watatu tulikalishwa katika kibanda kile cha walinzi tuingojea polisi kuja kutuchukua. Kila mmoja alikuwa kifua wazi akitikisika kwa hofu pia kutokana na baridi lililokuwa likitutafuna usiku ule wa saa tisa. Fikrani niliwaza namna ya kuepuka kadhia ile. Kulikuwa na jambo moja tu katika eneo hilo. Ilikuwa tufikishwe polisi ambako tungechukuliwa hadi mahakamani kwenda kujibu mashitaka yetu. Nilijua ni lazima tulikuwa tunaswekwa jela bila kukawia.

Ilipogonga saa kumi na moja alfajiri, wakuu wa mgodi ule walifika kabla ya wafanyakazi waliolala migodini hawajatoka,

pia kabla hawajaingia wanaofanya kazi mchana. Nia yao huwa ni moja tu, nayo ni kukagua kila kitu ili waendao waende kupumzika kwa uhuru na wanaoingia waingie kwa usalama.

Mkuu wa operesheni na afisa kazi alipofika alipewa ripoti kutuhusu. Afisa kazi huyo alikuwa mzungu mwenye asili ya Amerika. Kwa kumkadiria umri wake ni miaka isiyofikia arobaini na isiyopungua thelathini na tano. Alikuwa mrefu, mwenye kimo kilichozidi futi saba.

Alipoyapokea maelezo kutuhusu na hatua kwamba yatupasa kwenda polisi, alikataa kwanza. Alitaka kwanza tupelekwe kwenye ofisi yake ambako kuna jambo alitaka kutuhoji. Tulipofikishwa alianza kuuliza maswali.

"Mmewakamata wakiwa sehemu gani?" aliuliza mzungu yule ambaye niliposoma kibao cha mezani kwake kilisomeka jina lake kuwa ni Ivan Grant.

"Walifika katika chumba cha uchenjuaaji," alijibu mkuu wa walinzi wale. Katika kitambulisho chake kifuani niliposoma jina lake alikuwa akiitwa Maguzu Masese. Alikuwa mtu mrefu kwa kimo, mweusi na mwenye sura iliyojaa makunyanzi. Muda wote hakutabasamu wala kukenua yakaonekana meno yake.

"Walikuwa wamechukua nini?" akauliza Grant.

"Walikuwa bado hawajachukua chochote..ila walikuwa katika hatua ya kufanya hivyo," Maguzu alijibu.

Grant alikaa kimya kwa muda akitafakari. Akamtazama Maguzu kisha akatingisha kichwa.

"Maguzu, niachie hawa nyoka," alisema Grant kwa kiswahili kibovu kisha akainama na kuanza kuandika katika shajara yake.

Mlango wa ofisi ya Grant ulifunga, tukausikia unagonga, kitasa kikajibana. Hapo ndipo Grant alinyanyuka akaelekea

mlangoni. Alishika ufunguo akaubana mlango kisha akauchomoa ufunguo. Moyoni nilipata mashaka baada ya mlango kufungwa. Nilijua kinachofuata sasa ni kipigo na pengine angetuua kabisa.

Grant alirudi mbele ya meza yake. Akasimama. Akatutazama kwa jicho la kifo. Alivaa sare za kampuni yao iliyomaarufu zaidi katika ukanda wa Afrika, zenye nembo ya kampuni hiyo. Alilifunua shati na kiunoni akachomoa bastola fupi nyeusi. Akaiweka mezani. Akaingiza mkono mfukoni na kutoa simu mbili na kuziweka juu ya meza. Hapo ndipo nikajua nia yake ilikuwa hasi. Hatua ya kutaka kutuhoji ilikuwa ngumu sana kuikabili kwani tayari bastola ilianza kutishia uhai wetu.

Alielekea kwenye rafu lililokuwa kando ya meza yake. Akalifungua. Nikaona anatoa mtaimbo na nyundo. Alitoa pia msumeno mdogo – vyote akaviweka mezani.

Nilimtazama miguuni akiwa kavaa viatu vizito, vya mgodini. Aliposimama aligeuka,

akaelekea kwa rafiki yangu, Frank. Alimshika shingo kama paka kisha akamnyakua na kuelekea naye kwenye kiti cha mbao kilichokuwa kando. Alimketisha.

"Nani aliyewatuma kuiba?" aliuliza Grant.

Hakuna aliyejibu.

Nilimkodolea macho kwa ujasiri nikitaka pengine aniulize mimi. Najua Frank na Kanan wasingeweza kumjibu Grant kwa ufasaha na kuugusa moyo wake. Hawakuwa na sanaa ya kuzungumza kama mimi. Aliponiona nimemkazia macho alipiga hatua kunifuata. Mkono wake uliokuwa mkakamavu kama mkono wa kijiko cha kusawazishia barabara ukanishika shingoni. Akaninyakua kama mwewe abebavyo kifaranga. Akauliza, "Unaweza sema, nani kawatuma?"

Nilinyanyua kichwa nikatazama ukutani badala ya kumjibu. Macho yangu yakakwama ukutani, mahali palikuwa na kalenda yenye picha ya watoto wengi wa

familia maskini wakiwa wanapokea msaada wa chakula kutoka kwa Grant. Naye alibadilisha uelekeo wa macho yake. Akatazama ukutani.

"Unataka kusema nini?" akauliza. Akawatazama pia wenzangu ambao sasa walikuwa na manyunyuyu ya machozi machoni. "Niambieni, nani kawatuma kuiba?"

"Njaa!" nilijibu kwa sauti dhaifu.

"Njaa!" alistaajabu Grant. Akacheka kwa kejeli. "Kima nyie, nitawaua halafu niwazike chini ya msingi na nijenge choo cha maskini wenzenu juu yake!"

Mzungu yule alikuwa anakijua Kiswahili kiasi kwamba nilibakia namshangaa tu. Lafudhi yake ya kizungu bado ilikuwa ikisikika, lakini hakukosea kutamka neno. Nilipata mshituko kwa maneno yake ya kukera. Bastola yake ilikuwa mkononi sasa. Akaijaza risasi kisha akamfuata Frank na kumwegeshea shingoni.

"Niambieni — nani kawatuma?" aliuliza tena Grant. Sasa sauti yake ilikuwa na ukali usio na masihara hata kidogo. Nikaiona sura yake katika taa zile kali imevaa jazba. Mishipa ilijitandaza usoni na ikapotelea kichwani. Alipopumua nikaona kifua chake kinapanda na kushuka mithili ya puto lijazwalo na kutolewa upepo.

Haraka nilimgeukia. Ilikuwa lazima niseme, nimtaje ambaye hututuma. Nikawatazama wenzangu kwani uamuzi wa kulitaja jina la aliyekuwa akitutuma ni kununua kifo kingine. Alishatulisha kiapo kuwa siku tukikamatwa tuiseme hata kama tutauawa, lasivyo yeye angetufuta katika uso wa dunia kwa risasi moja tu.

Nilipowatazama wenzangu nikabaki na maneno yangu kooni. Nikamtazama Grant. Alinikazia macho na kunitaka kwa ishara nizungumze. "Sema!" alifoka.

"Kizito!" nikatamka jina hilo taratibu na kwa makini zaidi. Vinyeleo vya mwili wangu vikawa kama vimechomwa moto

jinsi nilihisi kosisimka kwa hofu. Ilikuwa vigumu kusema. Si vigumu tu kwa maana kwamba jina lilikuwa halitamkiki. Ugumu ni kulitaja jina la mtu aliyetulisha kiapo ambacho kufutika kwake ni kwa risasi ya moto. Achana na hilo, ugumu ulikuwa ni kumtaja mtu mwenye cheo – waziri wa nchi kitengo maalumu cha usalama wa raia. Lakini nilipuuza yote – hivyohivyo nilisema.

“Kizito yupi?” akauliza Grant.

“Mbunge wa eneo hili! Yule waziri.”

“Mheshimiwa Kizito, huyu waziri wa nchi katika idara ya--ehh?”

“Ndiye!”

Grant akageuza kichwa kisha bastola yake akairejesha mahala pake kiunoni. Akavuta pumzi ndefu na kuzishusha. Bila shaka nilipomtazama alikuwa akijaribu kukumbuka jambo, lakini akatingisha kichwa. Akanivuta. "Wewe njoo unieleze kwa kina."

Aliniketisha kwenye kiti kisha naye akavuta kiti kunisogelea.

“Nieleze, huwa anawalipa nini?”

“Chakula.”

“Unanidanganya!”

“Nasema kweli kabisa.”

“Chakula tu?”

“Ndiyo.”

“Mshaiba mara ngapi?”

“Mara nyingi.”

“Wapi huwa mnapeleka?”

Nikabaki kimya kwanza nikitafakari. Nikakikumbuka tena kile kiapo cha Waziri Kizito kuwa, siku tukimtaja na kuonyesha mahali na namna huwa anapokea mzigo wa mchanga atatua kwa mikono yake. Sikujali, ila niliamua kusema. Msemakweli mpenzi wa Mungu, hata kama nitakufa basi nife nimetapika ukweli wote. Nilitaka kufa kama shuhuda wa kweli aliyedhikika na kukongoka. Najua dhiki ilikuwa bwana

wangu wa kuniamuru nitende jambo au nisitende. Dhiki ile ile ilikuwa ikitoa amri kuwa kiungo changu fulani kitende jambo nilitenda. Sasa kusema ilinilazimu kwa sababu dhiki ni ileile. Hata kama nisingemsema Waziri Kizito, Grant alikuwa tayari kunitwaa kaburini kwa bastola yake sababu ya dhiki yangu. Dhiki ilinilazimisha kusema. Nikamtaja Kizito.

“Huwa anakuja na gari lake hadi nje ya uzio.” Nikanyosha mkono na kukifungua kidole changu kuelekea mahali ambako huwa tunapakia viroba. “Na hapo hubeba mifuko yote kwenye gari na hatujui kule huwa anaipeleka.”

“Yeye mwenyewe?”

Grant akameza funda la mate kulilainisha koo lake lililokauka sababu ya maneno aliyokuwa akiyasikia na kuyangojea yatoke zaidi.

"Ndiyo—ni yeye mwenyewe, wala si dereva wake."

Grant akasikitika sana. Umio katika koo lake likapanda na kushuka. likafanya hivyo mara idadi isiyoweza kuhesabika. Akawaza kwa muda kisha akatutazama kwa masikitiko. Mara hii akatulia kama mwenye kuingiwa na jini la ukimya.

“Mnapajua anapoishi?”

“Hatujui!”

Grant akachukua simu yake na tukaona anapiga. Simu iliita ikawa haipokelewi. Baadae ikapokelewa. “Naomba kuongea na Kizito!”

Hatukujua kilichoendelea baada ya hapo. Nilichoshuhudia ni Grant kuongezeka jazba na kuongea maneno ambayo sikuyasikia bayana. Lakini alighafilika sana. Alipiga simu tena kwa Maguzu akamtaka afike ofisini. Maguzu akaamrisha atuchukue huku akisindikiza msafara wetu kwa maneno. “Mkifika kituoni msemi ukweli. Msemi kama mlivyosema. Haiwezekani kiongozi mkubwa kama yeye awatumie

masikini kama nyinyi kuhujumu mradi wetu."

Ukawa wakati mgumu zaidi wa kwenda kumtaja Mheshimiwa Kizito katika dawati la mpelelezi wa polisi. Wakati tunapanda gari la Maguzu, kwa ghafla mno tukalionga gari la Mheshimiwa Kizito likisimama mbele yetu. Akatoka kwenye usukani. Nilipomtazama kwa makini, ile hali ya kutabasamu na kufurahia nasi haikuwepo tena. Sura yake ilifubaa, akawa kama amelishwa ndimu. Nikamchungua mkononi na kuona kashika bastola waziwazi. Ilikuwa saa kumi na mbili wakati wa pambazuko. Na huo wakati nikahisi utakuwa wa mwisho kuendelea kuivuta hewa ya bure japo kwa dhiki tele. Nikaona jinsi Waziri Kizito alinuia kutufuta duniani kwa risasi kama alivyokuwa kaahidi.

Nilipokuwa nimeketi nikaanza kujificha ili risasi isiye kuanza kutoa hukumu kwangu. Si kwamba niliogopa kifo, la hasha! Nilikuwa tayari kufa, ila namna ya kufa

bado sikuwa nimeijua. Sikuwa tayari kutangulia na nilihisi maumivu ya kifo kile baada ya risasi kuruhusiwa kunifuata yangukuwa makali sana. Kimoyomoyo nikaomba nife kifo chema. Macho yangu na ya wenzangu yote yakaelekea kwa Kizito.

Hakuna aliyefungua mdomo zaidi ya kubutwaa.

4

Nilisikia milio ya risasi na kemeo kwa ghafla mno. Kemeo zikafuatiwa mara kadhaa na milio ya risasi ya kuogofya. Nikajikunyata kama paka na kutamani hata sakafu ya gari lile la wazi ingepasuka inimeze. Mbali na milio, nikaona cheche za moto zikitokeza katikati ya misugvano ya boneti la gari la Kizito na risasi.

Nikaukumbuka ukatoliki wangu niliokuwa nimeurithi kwa wazazi wangu. Japo niliutelekeza miaka mingi nikimtumikia ibilisi kwa sababu ya dhiki, sasa nilirejea ibadani. Nikamwomba Maria mwenye heri, mtakatifu Yosefu na Yesu mwenyewe kuwa aingilie kati.

Sikukumbuka kutubu kwa ajili ya wizi zaidi ya kuomba ulinzi wa haraka.

Kilitokea cha ajabu mno, hata sikuamini tena kama Yesu na Maria pia Yosefu watanisaidia kwa wakati. Nikakumbuka mizimu ya babu zangu hata ambao sijawahi kuwaabudu hata mara moja—nao nikataka wawe wokozi wangu. Haikuishia hapo, nikarukia kwa Mtume Mohamamed mja mwenye heri kupitia maajabu yake huenda afike haraka niokoke. Bado mashaka yalinizidi moyoni. Nisingeishi pasipo kuwakumbuka wazazi wangu mahali pale. Nikamkumbuka baba yangu kipenzi na mama yangu niliyempenda mno, wangekuwepo huenda wangejaribu japo kunitetea nisitoweke duniani bila kelele. Lakini nao hawakuwepo.

Moyo wangu sasa ulifurika mashaka. Kelele za hapa na pale nikazisikia kila upande. Kilichonishangaza ni kuliona gari la mheshimiwa Kizito likirudi nyuma kwa kasi huku vioo anavifunga. Likakohoa

sambamba na risasi zile. Lilibvyogeuka nikaishia kuona moshi mzito kisha ukafuata mweusi na ngurumo kama za simba mwenye njaa. Likatoweka machoni huku nashuhudia kwa nyuma jinsi polisi walifunga kasi kwa nyuma wakilifuata.

"Bahati yenu—mngekufa hapahapa leo!" nikasikia askari mmoja anasema. Bunduki yake aina ya SMG ilikuwa mkononi ikitoa moshi uliokuwa wa kinyonge baada ya risasi zote kukosa shabaha.

Ningali nashangaa na kufunikwa na wimbi la hofu, askari yule alitingisha kichwa. Akaitua silaha yake chini na kuiachia ilale mchangani. Alipiga hatua akashindwa. Nikasikia analalama na punde akajikuta anachutama na kuketi mchangani. Kwa kumkagua kwa macho ningali ndani ya gari, niliona damu ikijitokeza taratibu kutoka upande wa kulia wa kifua chake. Na muda huohuo alilala chali na kutulia.

Sijawahi kuona askari akitokwa damu kifuani namna ile tangu nizaliwe. Sijawahi

kuwaza kama shujaa aliyevaa sare za jeshi la polisi, yenye nembo ya bendera ya taifa akapigwa risasi na kuuawa kizembe namna ile. Nikaingiwa uchungu kwa kumhurumia askari yule ambaye dhahiri alikuwa anakufa kifo cha kinyama. Alikuwa kazini akitetea uhai wetu, sasa yeye uhai wake ukawa sadaka kwa sisi ambao hata hatukuwa na thamani.

Askari baadhi ambao hawakuondoka na gari la polisi kumfuata Kizito walimsitiri askari yule. Nilipowatazama nilijionea nyuso zao zikiwa zimejawa giza la tanzia. Lilikuwa jambo gumu kuukubali ukweli wa muda ule. Kuona mwenzao anakufa mbele yao, tena akiuawa na mtu adhaniwaye kuwa mhalifu—haramia wa raslimali za watu ambazo askari walilenga kuzilinda naye akiwa ndiye kiongozi wa ulinzi kimamlaka. Japo askari wale walikuwa na roho za paka, katika nyuso za baadhi yao niliona machozi mepesi yakichomoza na kuchururika mashavuni. Lakini kwa ujasiri mkubwa kila

mmoja aliyafuta machozi. Vifua vyao vikavimba kwa hasira.

Waziri Kizito alichotaka ni kutuangamiza haraka kwakuwa tulikuwa tunaelekea kutoa ushahidi ambao hakika ungemchafua na kumfanya apoteze wadhifa wake. Nia yake ilikuwa atuangamize mapema ila akawa kawahiwa na askari ambao hakutegemea kama wangetokezea namna ile. Kwa bahati tu, risasi alizoruhusu kutufuata zilimfikia askari aliyekuwa kasimama kando ya gari la Maguzu, ambapo alikuwa kama katuziba tusifikiwe na mvua ya risasi zile.

Katika kituo cha polisi tulifungiwa kwenye chumba kidogo kilicho kichafu. Ndani tukawa zaidi ya watu wanane wenye kutuhumiwa kwa mambo mbalimbali. Hatukuwa na kauli yoyote zaidi ya kujawa na hofu ya kuuawa. Niliinama na kutafakari mengi juu ya maisha yangu. Nikayafikiri

maisha ya kwenda jela na umri wangu mdogo ingekuwa ndio mwisho wa ndoto zangu. Fikra zangu kuwa siku moja nitakuwa na kampuni kubwa ya TEHAMA ilianza kutoka kichwani taratibu. Nilianza kujiona katikati ya wafungwa watukutu. Sikujua idadi ya miaka ambayo mahakama ingetuhukumu baada ya kutukuta na hatia. Habari za kuswekwa gerezani ndizo zikatawala fikra zangu.

Wakati natafakari hayo, ilikuwa mchana wa jua kali tangu tukamatwe alfajiri. Habari za Waziri Kizito sikuwa nimezipata popote. Siku hiyo kulikuwa na shaka kuwa hatutapelekwa mahakamani wala hatutahojiwa kwani niliona askari wakiwa wima kila mmoja na jambo lake.

Lakini tofauti na matarajio kuwa hatutahojiwa siku hiyo, tulihojiwa mmoja baada ya mwingine. Wakahojiwa rafiki zangu kila mmoja peke yake. Zamu yangu ilipofika niliitwa. Niliingizwa ndani ya ofisi ya mpelelezi nikiwa sina kizuizi mkononi.

Nikaketi katika benchi lililokuwa kando ya meza ya mpelelezi. Akaanza kunihoji.

"Kwanini mlikwenda kuiba mgodini?"

"Njaa!" nilirudia jibu langu lilelile ambalo jana yake nilimweleza Grant.

"Mnauza wapi mchanga huo mkiuiba."

"Kwa Waziri Kizito!"

Mpelelezi akabaki kimya kwa muda. Akanitazama kwa jicho la mzaha.

"Mmeambiana mtoe jibu linalofanana?"

"Hapana afande. Kila mmoja anasema ukweli anaoujua."

"Kwanini unamtaja Waziri Kizito?"

"Ndiye aliyetutuma."

"Leo ilikuwa mara ya ngapi?"

"Inaweza kuwa ya nne au ya tano."

"Unao ushahidi kuwa Kizito ndiye anayehusika kuwaagiza?"

"Ndiyo."

"Ulishaonana naye au kuna muwakilishi wake?"

"Yeye mwenyewe."

Mpelelezi yule akabakia kimya kwa muda. Akachukua simu yake ya mkononi akawa kama anatafuta kitu ambacho sikukijua. Baada ya muda nikaona anaiweka simu sikioni. Akaanza kuzungumza.

"Nimepiga mara kadhaa simu yake haipatikani."

Nikabaki njiapanda sijui ambaye alikuwa akiongea naye.

Akakata simu.

Baada ya muda mfupi kabla hajaendelea kunihoji simu yake ikaita. Akaipokea.

"Ndiyo!" akasema mpelelezi.

Nikasikia sauti inatoroka katika simu yake hadi ikanifikia. Aliyekuwa akiongea alitoa taarifa ndefu ambayo iliweka umakini wa mpelelezi. Nikajikuta nabaki peke yangu ndani ya chumba kile kwa maana mpelelezi aliondoka. Nikaanza kusikia taharuki imezidi katika kituo. Gari la polisi lililokuwepo nikalisikia linapasha joto injini.

Akaja askari mmoja ofisini kwangu na kunichukua kunirudisha waliko wenzangu.

Mlango ulifungwa, na askari yule akaondoka. Nikaona analikimbilia lile gari na akachupia humo wakati likiwa limeanza kuondoka. Wakatokomea na kutuacha tukiwa na maswali lukuki. Tuliulizana maswali ya hapa na pale lakini hakuna hata mmoja ambaye alikuwa na jibu sahihi. Semasema yetu ilikatishwa na askari watatu waliofika kutuchukua wakiwa na nguo za kiraia. Walifika ghafla mno kiasi kwamba sote tulistaajabu sana. Kila askari mmoja akamchukua mtu wake. Mimi nilikuwa nyuma ya rafiki zangu. Sasa tulipelekwa kwenye chumba cha mahojiano tofauti na kile cha mpelelezi. Humo tukafungwa katika nguzo zilizokuwemo. Nilifungwa kwenye nguzo moja iliyokuwa karibu na ukuta na wenzangu wakafungwa kwenye chuma lililokuwa paani wakaning'inizwa kichwa chini miguu juu.

"Mnafanya tuonekane wazembe katika kazi zetu. Sisi hatuna muda wa kuwahoji ila tunataka msemi kila mmoja kwa uwazi. Kwanini mnamsingizia Waziri Kizito?" akahoji askari mmoja ambaye alikuwa mnene na tumbo lake lilikuwa limetangulia kwa mbele.

Niliingiwa hofu upya baada ya kuona kila mmoja kashika fimbo kubwa na nene. Mara nikasikia mlio wa fimbo ukifuatiwa na kilio kikali kwa mmoja wa rafiki zangu. Bila kusubiri nilitamka kwa sauti ya juu, "Nitasema kwa niaba yao."

"Sema haraka!" akafoka askari ambaye alikuwa karibu yangu. Nilisema yaleyale ambayo nilimweleza Grant kule mgodini. Askari wale hawakunisikiliza, zaidi waliendelea kusesitiza nimtaje mhusika tofauti na Kizito. Walidai kuwa kwa hadhi yake asingeweza kufanya mchezo huo wa hatari huku akiwa na uwezo mkubwa kifedha. Wakatoa picha tatu na kunionesha ili nimtambue Kizito kati yao. Picha

iliyokuwa kulia kwake ilikuwa ya mtu mrefu ambaye alivaa suti za rangi ya buluu, kiatu cheusi na miwani. Alikuwa na hadhi kubwa kwa mwonekano wake. Ya kushoto ilikuwa ya mtu aliyevaa suruari ya kaki, viatu vyeusi na fulana la kijani. Alikuwa na mwili mkubwa japo hakuwa mrefu kama yule wa kwanza. Sura ile nikaitambua. Ndiye Waziri Kizito ninayemfahamu na niliyekuwa namfahamu kwa kutambulishwa siku anatupatia kazi ya kusaidia kuiba mchanga wa dhahabu.

Sikusita kumtambua kwa kusema picha ile ya kushoto ndiye waziri Kizito. Askari wale waliangua kicheko na hapohapo wakaanza kunishushia kipigo kikali. Wakaniambia kuwa Waziri Kizito si lofa kama mtu yule tuliyemtambua. Hivyo hatumjui hata aliyetupa kazi ile kwakuwa tulikuwa tunadanganya.

“Acheni kuchafua watu—Waziri Kizito akijua mmemtaja hapa hakika mtajuta kuzaliwa. Nilipigwa kwa kiasi kikubwa hadi nikahisi

kupoteza fahamu. Kipigo kile pia kilitishia uhai wa rafiki zangu ambao walikuwa hawajiwezi.

Baada ya fahamu zangu kuanza kuhama, kwa mbali nilisikia askari wakiteta kuwa wahitimishe safari yetu hapa duniani kwani tutakuwa wasumbufu siku za usoni kutokana na usugu ule. Askari mmoja akasema, "Hawa tuwatie katika viroba, tukawatupe ziwani. Wakikua hawa watakuwa majambazi sugu na tutateseka sana kwa kuacha usingizi wetu kuwasaka wakiwa wamefanya matukio makubwa."

Sikuwa na uwezo wa kukimbia kwani mwili ulikaribia kutengana na roho, ila nilisikia. Ningefanyaje kama dhiki ilinifikisha mahali pale bila hiari yangu? Nikabaki kimya nikiamini Mungu pekee ataamua hatima yetu.

Wakati wa usiku tuliviringwa kwenye turubai badala ya kutiwa katika viroba. Hatimaye tukabebwa na gari iliyotuchukua hadi ziwani ambako tulitupwa wakijua sisi ni wa kufa tu baada ya kipigo walichotupatia.

5

Asubuhi jua lilikuwa limechomoza. Sote tulikuwa bado wazima—hakuna hata mmoja aliyepoteza maisha katika jaribio lile la kutuua tukiwa katika boti iliyokuwa katikati ya ziwa. Kilichokuwa kimetokea ni kibaya sana. Kabla ya tukio lile kutokea mvuvi mmoja aliyekuwa katuokota katika ufukwe wa ziwa alituambia, “Ingieni kwenye turubai mlale kabisa maana mawimbi ya ziwa ni makubwa.”

Maneno ya yule mzee yakanishangaza. Nikataka kubisha kila nilipotazama ziwani—hapakuwa na mawimbi na maji ya ziwa yalikuwa tulivu.

“Mbona ziwa liko tulivu mzee!”

“Nionacho mimi ni tofauti na macho yenu. Fuata nilichosema!” akakazia kwa kufoka. “Au mnataka niwatose ziwani?”

Bado sikuona uhusiano wa mawimbi makubwa na sisi kutakiwa kulala. Nikawatazama wenzangu. Frank akalala na kujifunika turubai. Kolan yeye alibaki kuangaza macho kila upande na mwisho naye akajikuta anajichimbia ndani ya turubai. Nilibaki naangaza macho ili niyaone mawimbi aliyoyasema yule mzee. Sikuyaona. Nilipomtazama mzee yule kwa makini nikaona anakoelekeza macho. Kulikuwa na boti moja ikienda kasi sana. Mara ile nilipoona ikiyaparamia maji nikajifunika turubai na kufunua sehemu kidogo ambapo jicho langu moja lilikuwa linamwona yule mzee na kuona kwa mbele tuendako. Nikamwona yule mzee anavuta mfuko wa sandarusi uliokuwepo kando yake huku akiendelea kuiongoza ile boti.

Kila sekunde jicho lake likawa nyuma na likarudi kwenye kile kiroba. Mara nikawa nasikia ngurumo ya injini ya boti iliyokuwa nyuma yetu na ndipo nikaona mzee yule amechomoa bastola kutoka katika kile

kiroba. Moyo wangu nikahisi unakosa utulivu. Mapigo ya moyo yakaufanya mwili wangu kutingishika kwa hofu.

Kwa ghafla mno ile hali ya kukumbuka madhara ya ile bastola yakanijia tena kwa kukumbuka tukio la kutaka kuuawa kule shambani kwa Bupe. Nikasafiri tena mbali hadi mahali familia yangu iliagamizwa pamoja na mbwa, wetu Shilata. Kwa namna nilikuwa namchukulia yule mzee sasa nikamwona ni hatari zaidi. Nikajua huenda alikuwa akifanya kazi pamoja na polisi— kwa maana walitutupa pale ili aje atuchukue na kutupeleka mahali ambako tungeuawa bila hata woga wowote. Au la, nilihisi pengine angetuzamisha majini katikati ya ziwa na tupoteze maisha kwa maji.

Haikupita muda nikasikia milio ya risasi ikinguruma. Kila mmoja akataharuki. Nikafunua kiasi kikubwa cha turubai ambapo niliona waziwazi jamaa watatu kwenye boti iliyokuwa inatufuata wakiwa

na bunduki nzito za kivita. Yule mzee jasho lilikuwa likimtoka na ndipo nikatambua kuwa hakuwa mzembe kwa kiasi kile. Risasi za bastola yake zikawatafuna watu wawili waliokuwa wakimshambulia na kwa macho yangu nikawaona wanamezwa na maji ya ziwa. Boti yao ikafuka moshi mzito baada ya kupoteza njia na kuliparamia jiwe. Kwa ghafla mno ilisimama na kuanza kumezwa na maji.

Boti aliyokuwa nayo yule mzee ilishika kasi kuelekea mahali ambako sikuwa napaona mwisho wake. Nikitazama niliona maji matupu yakimetameta katikati ya mwanga wa jua lililokuwa linachomoka kwa kasi kutoka mawinguni. Ilituchukua takribani saa tatu tukiwa majini kwa safari ambayo sikujua tunakoelekea. Sikuwa na namna ya kufanya—hata kama kumtoroka yule mzee ilikuwa si rahisi kwa maana sikuwa najua kuogelea, hata Frank na Kanan walikuwa kama mimi. Hata hivyo, kwa kile kipigo cha polisi tusingeweza kufanya

chochote kwa maana maungo yalikuwa yamelegezwa kwa virungu vya polisi.

Hatimaye boti ilipotia nanga mara moja kuna vijana wanne walifika hadi kwenye boti. Wakiwa bado wamestaajabu wakitushangaa mzee yule akawapa amri, “Shusheni samaki, pia washushe hao!”

Mazingira ya mahali pale yakabadilika ghafla mno. Wale vijana wanne ambao walikuwa wakituzidi kwa umri hawakushusha samaki. Walitushusha mmojammoja na kila mmoja akachukuliwa hadi kwenye kibanda akafungwa kwenye nguzo iliyochimbiwa. Tukafungwa kwa kuzungushiwa kamba mwili mzima—kutokea miguuni hadi shingoni, kama joka lifanyavyo wakati wa kufunga windo lake ili lilainike. Hata sura za watu wale hazikuwa na bashasha.

Cha kushangaza hatukumwona tena yule mzee. Kila nikivuta kumbukumbu mara ya mwisho nilimwona mzee yule akiingia kwenye moja ya hema lililokuwepo mbali

kidogo na kibanda tulichokuwa tumefungiwa. Sikumwona kutoka katika hema hilo. Yamkini alilala kwa sababu ya uchovu aliokuwa nao.

Kufungwa mahali pale kwa mtindo ule ilikuwa dalili mbaya kwamba tulikuwa bado mikononi mwa watu wabaya. Akilini sasa ikanijia fununu ya kuwa kuna watu hutekwa na kuuzwa kwa makundi ya kigaidi, na wengi hutolewa visiwani katika ziwa hilo kubwa. Fikra hiyo pia ilikuwa nafsini mwa wenzangu pia—maana Kanan na Frank walisema waziwazi kuwa sasa tunaenda kuwa watumwa katika makundi ya kigaidi.

Wakati tunawaza hayo, kuna boti moja ilitia nanga katika ufukwe wa kisiwa kile kidogo. Akashuka mwanaume mmoja mrefu, mwenye mwili mkubwa na mkakamavu. Wakampokea vijana wale kwa heshima kubwa hata nikastaajabu. Moja kwa moja akaenda hadi kwenye hema alikuwa kaingia yule mzee. Nikawaambia wenzangu

kuwa, yule mzee atakuwa katuuza kwani yule jamaa aliyefika lazima atakuwa mnunuzi. Na sasa kilichokuwa kikifanyika ni kupatana bei na akilipa tu, lazima tutachukuliwa tuondoke naye.

Kweli. Baada ya kama dakika ishirini wakiwa ndani ya hema, walitoka. Moja kwa moja mzee yule aliyetuokoa katika ufukwe akaamuru tufunguliwe. Tuliingizwa kwenye boti ya yule mgeni. Tukahifadhiwa katika makasha makubwa—kila mmoja ndani ya kasha lake. Boti iling'oa nanga kutoka eneo lile tukiwa tumeshajua kuwa tayari tuliuzwa kwa kundi la kigaidi. Hatukuwa na namna ya kujitetea kwani tulikuwa taabani tumeumizwa na virungu pamoja na njaa ya siku mbili bila chakula.

6

Boti ya mtu ambaye alituchukua ilitia nanga kwenye gofu la meli kubwa iliyokuwa ikielea ziwani. Kwa namna ya pekee ile fikra ya kwamba tulikuwa tunachukuliwa kwenda utumwani kwa magaidi ilizidi kuchipua fikrani mwangu. Tukatolewa kwenye boti na watu wanne waliokuwa katika meli ile. Watu wale hawakutusemesha lolote. Tuliingizwa ndani ya meli ile ambamo tulipewa chakula na matibabu ya hapa na pale. Meli ile ilionekana kama gofu kwa nje lakini kwa ndani ilikuwa na mazingira mazuri—ikiwa na ofisi na vyumba vya mazoezi.

Katika meli ile tulikaa juma zima tukipatiwa matibabu na kufanyishwa mazoezi mepesi na magumu kwa ajili ya kuiweka miili yetu sawa. Tulipoanza juma

la tatu miili ilikuwa imara na ndipo siku ile tuliitwa kwenda kwenye ofisi moja ambayo nayo iko ndani ya meli ile. Tulikuwa na wasiwasi kila wakati kwani sote tulihofu kuchukuliwa na kwenda kuwa watumwa wa magaidi waliotapakaa duniani.

Tuliingia ofisini na kukuta chumba cha ofisi kikiwa na viti vitano. Viti viwili vilikuwa nyuma ya meza na vitatu vikiwa mbele yake. Meza haikuwa na kitu chochote. Aliyetuchukua akatuamuru kuketi. Tukaketi.

Tulibakia katika hali ya ukimya tukitazamana. Na baada ya kama nusu saa tukaona askari mmoja anakuja akiwa kavaa sare za kijeshi. Mkononi alibeba kibegi kidogo ambacho alikiweka mezani. Alitoka. Tulikuwa watulivu hadi tuliposhuhudia watu wawili wanakuja ndani ya chumba. Waliketi katika viti wakawa wanatukabili. Sura zao hazikuwa ngeni hata kidogo, ila ni yule mzee aliyetuokota kule ufukweni tulikotupwa na polisi. Mtu wa pili alikuwa mwanaume mrefu ambaye alituchukua

kutoka katika kisiwa ambacho mzee aliyetuokota alitupeleka.

Walitutazama kila mmoja kwa wakati wake.

“Ni kwa kipindi kirefu tangu niwaokote hatujaongea lolote. Sikutaka kuongea nanyi kwa sababu nilitaka kwanza afya zenu ziimarike. Sasa ndio wakati wa kujuana vema kabla ya kuchukua uamuzi wowote juu yenu,” alisema mzee aliyetuokota. Mwenzake alikuwa akitingisha kichwa kukubaliana naye.

Tulipewa maelezo mengi na mzee yule kuwa yeye ni mvuvi wa siku nyingi. Na maisha yake yote ni ya kuishi visiwani hivyo kila mmoja alipaswa kueleza wasifu wake. Frank alieleza wa kwanza historia yake iliyojaa uchungu, kisha Kanan alijitambulisha naye kueleza wasifu wake. Maisha yao wote yalikuwa ya kusikitisha. Frank hakuwa anawajua wazazi wake kabisa. Kwa mujibu wa Frank ni kwamba, angali kichanga alilelewa katika kituo cha

yatima hadi alipofikia umri wa miaka sita ndipo alitoroka na kuingia mtaani. Alianza kuishi maisha ya upweke katika stendi ya mabasi. Hadi nakutana naye akiwa na umri wa miaka kumi alikuwa kaizoea mitaa yote ya jiji la Mwanza.

Kanan yeye alijieleza kuwa maisha yake yalianza kwenda hovyoy na kukimbilia mtaani akiwa na miaka minane. Wazazi wake walipata ajali ya treni maeneo ya Msagali na kupoteza maisha. Baada ya ajali, wajomba zake walianza vurugu na harakati za kuwadhuru. Walimuza dada yake ambaye alikuwa mdogo kiumri akachukuliwa na watu wasiojulikana na kupelekwa kusiojulikana. Hapo ndipo Kanan alipokataa kununuliwa na alitoroka. Akaanza maisha yake mapya kwa kujifichaficha mtaani huku akiwindwa. Kwa maana hiyo, Kanan alikuwa mkubwa kwa umri kumzidi Frank.

Nilieleza historia yangu ilivyokuwa mwanzo hadi tulipokuwa tumeshikiliwa na

watu tusiowajua. Historia zetu sote zilikuwa za kutia uchungu mno. Kwa kifupi, sote tulikuwa wahanga wa matatizo ya kijamii na tulipoteza familia zetu na kuwa wageni wa mitaa iliyojaa dhiki. Sasa sote tulikuwa wageni kwa watu tusiowafahamu na mahali tusipopafahamu.

Ndani ya meli ile kulikuwa na pilikapilika za hapa na pale. Mbali na kuwa na kitengo cha afya na vyumba vya mazoezi, kulikuwa na sehemu ya wavuvi waliokuwa wakija na kutoka na boti zao. Wasiwasi wangu ukabaki mahali pamoja tu—ni kuhusu yule mwanajeshi aliyefika na kibegi na kukiweka juu ya meza. Nilikuwa pia nangoja kusikia lengo la kutuchukua na kuhangaika kote huko kwa watu wale baada ya kutuchukua.

Fikra zangu zikawa kama zimewachochea watu wale kuanza mazungumzo kwani sisi tulishatoa historia zetu mbele yao. Yule mzee akasema, “Mlipo hapa ni mahali salama. Kama

mlivyoshuhudia mazingira yangu yote, mimi ni mvuvi wa siku nyingi. Tukio la kutupwa na polisi kule ufukweni nililiona nikiwa nimetia nanga mbali kidogo na mahali pale. Sasa, ili tuendelee yafaa mueleze ni nini kilitokea?”

Nilieleza kila kitu kilichotutokea kwa watu wale. Na mwisho ndipo yule mzee akajitaja jina lake kuwa ni Amando— ambaye ni mwanajeshi mstaafu wa jeshi la wanamaji Tanzania. Alishawahi kuwa katika kikosi maalumu cha jeshi kwa ajili ya ulinzi wa nchi. Mbali na kujitambulisha, akamtambulisha mwanaume aliyekuwa mbele yetu, ambaye alituchukua hadi kutufikisha mahali tulipo—kwenye meli chakavu kwa nje ila ndani kukiwa na mazingira ya kuvutia. Akatueleza kuwa yule ni luteni wa jeshi la ulinzi, ambaye anahusika na operesheni maalumu za kijeshi. Yeye anahusika katika kutafuta na kuandaa makomandoo kwa ajili ya misheni pamona

na Oparesheni maalum. Akasema, “Hapa ni ofisini kwake na yupo kazini kwa saa 24.”

Nilistaajabu na hapohapo nikabaki na maswali mengi kichwani. “Amando alinipigia simu na kunieleza jinsi aliwapata. Sasa, kwakuwa maelezo yenu yanaonesha kuwa mnastahiki kutengenezewa maisha yasiyo ya kubahatisha, niliamua kuwawezesha,” alisema luteni yule ambaye jina lake kamili alijulikana kama Luteni Rado.

“Nimeshafanya uchunguzi kwa muda wote mliokuwa hapa, na nimebaini kuwa mliyosema yote ni ya kweli. Hadi sasa najua mtakua na moyo wa dhati wa kulitumikia taifa lenu katika idara mbalimbali. Ila, kwakuwa sasa tunajenga timu ya operesheni maalumu huenda mkasaidia hapo mbeleni. Operesheni zetu ziko nyingi, lakini hadi muive.”

“Ki-vipi mzee?” niliuliza.

“Kama mnaafiki kujiunga na kundi la vijana walio katika mafunzo kwa muda wa

miaka minane—basi mnatakiwa kujiunga mara moja. Tunalo kundi la askari vijana walioanza mafunzo rasmi katika bahari ya hindi wapatao ishirini na wawili. Mkijiunga nao mtakuwa ishirini na tano. Lakini, mwisho wa siku tunatarajia kuchuja na kubaki na vijana watano wa Operesheni maalumu. Na askari watakaoshindwa kuingia katika kikosi maalumu cha operesheni watajiunga na jeshi katika idara mbalimbali,” alifafanua Luteni Rado.

Hapo ndipo nilianza kutambua nia ya watu wale. Nikajikuta napata faraja taratibu kwani sasa nitakuwa na mafunzo ya hali ya juu, ambayo yataniwezesha kuwatafuta wauaji wa familia yangu na kuweza kulipa kisasi kirahisi zaidi.

Nilitabasamu. Amando aliponitazama akatabasamu pia. Luteni Rado naye aliponitazama nikaona anatingisha kichwa akifurahi. Akasema, “Jamshid nimekuelewa, pamoja na wenzako.” Akasimama. Akafungua mkoba wake na kutoa vitabu

vitatu. Kila mmoja akatupatia kitabu kimoja. Vilikuwa vitabu vyenye hadithi za wanajeshi waliofanikiwa katika misheni zao.

“Sasa, hivyo vitabu vitafungua uelewa wenu na hisia zenu kuhusu mambo ya kijeshi, uzalendo na umuhimu wa kuwa mwanajeshi katika taifa lako,” alisema Luteni Rado.

Usiku tulipelekwa bandarini, mashariki mwa ziwa. Tukachukuliwa na gari maalumu kupelekwa katika ukanda wa Bahari ya Hindi ili kujiunga na waliokuwa wanapokea mafunzo yatakayofanya wachaguliwe askari watano tu kujiunga na kikosi maalumu cha jeshi. Tulipofikishwa pwani, wakati tunangoja tulivamiwa na genge la watu. Tulitekwa na kupandishwa kwenye boti.

7

Mafunzo yalikuwa magumu. Kuimaliza miaka minane lilikuwa jambo gumu sana kwa namna niliona. Kuna wakati nilitaka kutoroka lakini kila nilipokumbuka jinsi waliuawa wazazi wangu, dada yangu na mlinzi wetu, pamoja na Shilata, sasa nilistahimili mateso ya aina yoyote. Sikukubali kushindwa. Nililikuwa na nia ya kuwa miongoni mwa askari watano watakaokuwa katika kikosi maalumu. Kanan na Frank pia walikuwa na ari ya ajabu ya kuzitaka zile nafasi tano. Nikakumbuka maneno ya Frank siku moja aliponiambia, “Nitakuwa miongoni mwa hao askari wa kikosi maalumu—tena nitakuwa kiongozi wenu!”

Nilicheka aliposema hivyo na kumwambia, “Wakati utaamua. Wakati ni

mwamuzi wa kila jambo, ila najua sote tutakuwa ndani ya kikosi kile.”

Mfululizo, kwa miaka yote tuliyokuwa mafunzoni, siku za jumamosi na jumapili zilikuwa za kufanya shughuli binafsi. Kuna wakati tuliruhusiwa kwenda matembezini popote ila isiwe mbali na kambi yetu ya siri iliyokuwa mwambao wa Bahari ya Hindi. Nilikusudia mwisho ule wa juma nitoke na kwenda jiji Dar es salaam kwa misheni maalumu. Nilitaka kwenda kufuatilia mambo ya familia yangu iliyolala. Nilitaka kujua mahali ambapo wazazi wangu walizikwa. Siku ya Ijumaa, ilikuwa usiku ndipo nikashikwa fikra ya kuwajuza rafiki zangu, Frank na Kanan kuwa kesho yake twende jijini Dar es salaam kwa ajili ya mambo kadhaa. Nilitaka wanisindikize lakini nilisita kuwajuza misheni yangu—ila ilitosha kwenda nao hadi yalipo makaburi ya familia yangu yote iliyoangamizwa kwa

risasi. Bado moyo wa kisasi uliendelea kufurukuta kwa joto kali. Hamu ya kuwajua wahalifu ilimea taratibu nafsini mwangu. Nilitamani sasa niwapate na niwape adhabu inayostahili. Ikanilazimu usiku ule kuwaita Frank na Kanan ili kuwajuza mpango wangu. Walipoketi nami niliwaambia, “Kesho nawaomba tutumie muda wa mapumziko kwenda Dar es salaam. Huko ninataka kwenda kuyaona makaburi ya ndugu zangu, na-na-” nikasita kusema.

Frank na Kanan wakanikodolea macho wakingoja niendele kuyasema niliyokusudia kuyasema.

“Sema tusikie!” akasema Frank.

“Hapana, nimemaanisha hayo tu,” nikamjibu.

“Si hivyo Jamshid—mimi ni kiongozi wako. Najua unachowaza. Hata ukificha mimi nishajua. Sauti yako imeficha kitu fulani nakisikia,” akasema Frank kama utani vile. “Au niseme?”

“Sema – nini?”

“Najua damu ni nzito kuliko maji. Kila amwagaye damu ya mtu asiye na hatia na damu yake pia humwagwa—hata kama kuna msamaha, nafsi ya aliyedhulumiwa huwa haisahau. Najua unataka kupeleleza ili angalau uwajue wauaji,” akasema Frank kwa kunipatia kabisa.

Nikatabasamu na kukubaliana naye kwa kutingisha kichwa. Muda huo nilifahamu kabisa kuwa rafiki zangu walizijua hisia zangu kabisa. Ila sikutaka kuwaweka wazi japo walikuwa wanafahamu.

“Sikiliza Jamshid....sisi ni ndugu zako japo si wa damu. Lolote unalotaka kulifanya tutalifanya sote kwa umoja wetu. Hata Frank akitaka msaada kwa jambo lolote mimi na wewe lazima tushiriki. Vilevile nikiwa na lolote mnatakiwa msimame kunisaidia. Tuko pamoja Jamshid—kwa lolote,” akasema Kanan.

Nilikaa kimya na kutafakari sana. Kwa hakika nikajikuta nawaeleza rafiki zangu

juu ya nia yangu. Nikamaliza kwa kusema, “Tutaanzia mahali tulipokuwa tunaishi, pia tutaenda makaburini na mwisho kuna mahali nilificha kadi ninayoamini itakuwa na ushahidi.”

“Mahali ulificha kadi?” akauliza Frank.

“Ndiyo.”

“Wapi?”

“Utapaona tukifika.”

“Una uhakika itakuwa bado nzima kwa miaka zaidi ya kumi na tatu?”

“Ninayo hakika — niliihifadhi mahali salama.”

“Sawa — tutakwenda pamoja,” alisema Frank. Cha kushangaza, wakati tunamaliza kufanya mazungumzo, nikasikia mtu akikohoa kando yetu. Nilipogeuka nikaona mtu akitokomea gizani na kuelekea sehemu ya giza nje kabisa ya kambi yetu. Frank, Konan na mimi tukasimama na kuanza kumfuatilia. Lakini akazidi kutokomea nasi tukazidi kumfuata machakani. Nikajikuta

natamani sana kumjua mtu yule ila Frank akatuonya, “Turudini. Tutakuwa tumewekewa mtego mahali huko.”

Tulirudi. Tukatoa taarifa kwa kiongozi wa kambi ambaye alitutaka kuongozana naye, pia akachukua wenzetu watano tukaenda hadi ufukwe uliokuwa upande wa pili wa Bahari ya Hindi, ambako mtu yule alielekea. Kadiri tulivyokaribia ndivyo wasiwasi ulizidi. Kila mmoja alikuwa na bunduki yake mkononi tayari tayari. Ufukwe ulikuwa kimya lakini tukawa tunasikia injini ya boti ikinguruma na maji yakipiga kelele. Hatimaye boti ile iliwasha taa na mwanga mkali ukaonekana. Ilikuwa mbali na mahali tulikuwa hivyo tukaishia kuiona boti inapotelea kwenye kilindi cha bahari.

Kamanda wa kikosi chetu alitutaka turudi kambini haraka, lakini cha kushangaza, kila tulivyopiga hatua kwenda kambini tulizidi kuhisi harufu ya sigara

ikipenyeza katika mianzi ya pua. Kila mmoja akataharuki.

“Mkuu—harufu ya sigara!” nilisema kwa wasiwasi niliokuwa nao.

Kamanda wa kambi yetu ya mafunzo akatoa amri.

“Kuna hatari huenda ikawepo.”

Kamanda akatoa amri kuwa kila mmoja kutokea mahali tulikuwa afuatilie ni mahali gani harufu ile ilitokea. Tukajipenyeza kila mmoja na njia yake. Kwa kuwa tulikuwa upande wa magharibi na kambi, na ndiko mahali upepo uliokuwa unavuma ulielekea, dhahiri kila mmoja alikuwa na dira ya kutafuta akielekea mashariki—kwenda mahali kambi yetu ilipo.

Sakasaka ile ikatuchukua dakika kadhaa pasipo kuona chochote cha kutilia shaka. Tukajikuta sote tunafika katikati ya kambi bila kujua mahali hasa ile harufu ilitokea. Kamanda wa kambi akateua wachache-ikiwemo mimi na Frank. Akatutaka haraka

tuongozane naye hadi ilipo ofisi yake na akatupatia king'amua moshi. Kifaa kile kilikuwa cha kisasa mno kwa maana kilikuwa kinatoa moshi kuelekea mahali harufu ya moshi ilitokea nasi tulikifuata kadiri kilivyoelekeza.

Kadiri tulivyokifuata ndivyo kilizidi kutupeleka ndani ya kambi, katika hema ambamo kuruti wa kikosi cha tatu walikuwa wakiishi. Tulipoingia ndani ndipo kifaa kile kikatoa mlio mkali na taa yake nyekundu ikawaka.

Ilikuwa hali ya hatari. Tulipopekua tukaliona bomu lililoteywa likaunganishwa na kamba ndefu ya mkonge iliyokuwa tayari imeloweshwa ikaunganishwa na moyo wa bomu la kutengeneza kwa mikono. Lengo la aliyelitega ni kuwa sigara ile ingewaka na katika kumalizika, moto wake ungetoa nafasi ya kamba ya mkonge kushika moto na kuupeleka kwenye bomu na kulifanya lilipuke.

Kwa muda huo hadi tunaona hatari ile, sigara ilikuwa imewaka robo tatu, na robo pekee ilikuwa imesalia. Hapakuhitaji utaalamu mkubwa kulitegua bomu lile. Frank kwakuwa alikuwa katika kitengo kile kwa muda, aliifyatua kamba ya mkonge kutoka kwenye moyo wa bomu na kuikunja kisha akakifinya kipande cha sigara kukitenga na kamba. Bomu lile lilichukuliwa na kuharibiwa usiku ule. Tukagawiwa katika makundi ya kufanya doria usiku ule ili kama kuna mtu yeyote yumo ndani ya kambi asitoroke bila kukamatwa.

Lakini katika hali ya kutamausha mno, upande wa pili wa kambi tulisikia milio ya risasi ya ghafla.

**Riwaya hii inaendelea hadi mwisho.
Ukitaka nakala ngumu weka Oda kwa**

1. NAMBA 0743 017 563 (SMS, DIRECT CALL)
2. NAMBA 0625 813537 (WhatsApp)

Nakala laini kitabu kizima kinapatikana kwa Tsh. 5000/=

Ukitaka kujiunga na group maalumu la kusoma riwaya zote mpya pamoja na hii unalipa Tsh. 3000/= kwa mwezi. Kutakuwa na riwaya 3 zinazoendelea hadi mwisho. Vigezo na masharti vitazingatiwa kwa wanaojiunga na kundi.

Share sample ya Riwaya hii popote na marafiki..bureeee.

**TAZAMA MACHAPISHO MAPYA KURASA ZIJAZO
10,000@ BOOK**

MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA

JOHN WISSE



Anayewinda..
anawindwa...mwendo
wa kuwahiana..

KISIRANI!

PAKA HAWEZI KUISHI KWA MSELA

MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA
JOHN WISSE




Misheni #5 **MOSCOW**

Risasi zimeisha, adui wanamwandama kama nyuki...
akikamatwa ni kifo...kilichobaki ni kupigania pumzi....
Raymond Chato sasa yupo shimoni...

MTUNZI #1 WABETA DAISTOPIA


JOHN WISSE

The book cover features a surreal landscape. In the center, a man in a dark suit is kneeling on a red, blood-like trail that winds across a light blue, textured ground. He is surrounded by tall, purple, grass-like plants. The background is a pale blue sky with faint, wispy clouds. At the bottom, there is a dark green, rocky horizon line.

PROPAGANDA


NIUENI MKITAKA, UKWELI WOTE NITASEMA


...Siusiushu wa taifa anabaini faili lenye siri nzito kuhusu mpango wa chanzo ya Korona. Y
tayari kufa akitea taifa lisiwekwe rehani. Sasa anahatarisha usalama wa taifa na wake
mwenyewe. Atafanya nini wakati anawindua kuuma?"



MTUNZI #1 WABETA DAISTOPIA

JOHN WISSE






Kachero wa kukodi, Raymond Chato anapaswa kumwoko a binti wa tajiri wa Kitanzania aliyenaswa katikati ya mapigano mjini Donboss. Je, ataweza wakati eneo lenyewe limejaa uasi na mauaji ya kila mgeni ndani ya mji?

MISHENI #4 UKRAINE

TUMAINI LIPO GIZANI



JOHN WISSE
MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA

(kumbukumbu ya mauaji)

walitaka
GIZA

wakaizima
NURU

John Wisse

MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA